

WASEMAVYO WASOMAJI WA KITABU HIKI

Mimi binafsi nimepata muda wa kusoma kitabu hiki. Nimejifunza siri kubwa katika maisha haya ambayo shetani hataki watu wajue nayo ni KUSAIDIA WAJANE NA YATIMA. Nimesoma vitabu vingi vimenisaidia sana na kunipa maarifa, lakini maarifa niliyopata katika kitabu hiki yatanisaidia nikiwa duniani na mbinguni pia. Faida za kusaidia wajane na yatima haziishii duniani tu bali hata baada ya maisha ya duniani. Kitabu hiki kinapaswa kisomwe na kila mtu ni muhimu sana.

Michael Severine Mwingira

Huston, Texas

Mfanya biashara

Hakika kitabu hiki ni kama sega la asali ni vigumu kulipata kwasababu linalindwa na nyuki wakali lakini ukilipata hakika utaona ladha na utamu wake. Shetani hatamani hata kidogo watu wajue Baraka zilizopo katika kusaidia wajane na yatima. Mwandishi ametusaidia sana kutufunulia siri hizo. soma kitab hiki utashangaa.

ABELLY MHAPA

KKKT-RUANDA MBEYA

TANZANIA.

Kitabu hiki kimenifundisha mambo mengi sana. Lakini jambo kubwa nililojifunza ni kuwa kamwe huwezi kufanikiwa ikiwa huna moyo wa kusaidia wengine. Maisha ni upendo. Kitabu hiki kimenifundisha kuwa ikiwa una mpango wa kufanikiwa hapa duniani na kwenda mbinguni pia basi huna budi kujifunza kusaidia wajane, yatima na wahitaji. Kusaidia wajane na yatima

*ni alama ambayo haifutiki mbele za Mungu hata kama
utaondoka Duniani. Karibu usome kitabu hiki.*

Mch: HARRIS KAPIGA

Mtangazaji wa Habari clouds Tv.

Mwandishi wa kitabu cha ubunifu.

*Maisha ni huduma. Tumezaliwa ili tuwahudumie watu
wengine hii ndiyo kanuni kuu ya maisha ya mafankio
duniani. Nyumba unayokaa kuna mtu alijenga, Gari
unalotumia kuna mtu alilitengeneza. Miti ipo ili
kutupatia sisi matunda na kivuli. Kitabu hiki
kimenifundisha mambo haya na mengine mengi. Soma
ujionee mwenyewe.*

IGNAS SWAI

MTANGAZAJI RADIO BARAKA-MBEYA

UTANGULIZI

Yapo mambo mengi sana ambayo ni muhimu katika maisha yetu, ambayo tunatakiwa kuyatekeleza kabla ya muda wetu wa kukaa hapa duniani haujaisha. Na ikiwa mambo hayo ya msingi hatutayatekeleza maisha yetu yote hapa duniani hayatakuwa na maana kabisa. Pamoja na majukumu mengi uliyo nayo katika dunia hii, hili jukumu usilisahau kabisa. Jukumu lenyewe ni kuwasaidia wajane, yatima na wasiojiweza. Biblia haimuungi mkono mtu yoyote duniani ambaye atatoa udhuru wa kutekeleza jukumu hili. Jambo hili si kwa mkristo tu bali ni kwa kila mwanadamu aliyejaliwa kuishi. Jambo hili limeonekana kama utumishi mdogo sana duniani lakini ni utumishi mkubwa sana mbele za Mungu. Mungu amenipa ujumbe huu nikufikishie sio kwa bahati mbaya hapana ni kwa makusudi kabisa. Unaweza kudhani ni bahati mbaya tu kitabu hiki kukufikia mkononi mwako la hasha ni makusudi kabisa ya Mungu ukipate ili ukisome na upate ujumbe huu. Usichoke rafiki jitahidi usome hakika utaelewa vizuri.

Jambo la kusaidia wajane na yatima sio jambo la hiari, hapana ni la lazima kibiblia. Zipo Baraka nyingi sana ambazo zimefichwa katika kusaidia wajane na yatima ambazo huwezi kuzipata kwa namna yoyote isipokuwa katika kuwasaidia wajane na yatima.

Zipo laana nyingi sana ambazo zitampata mtu yoyote ambaye hajishughulishi na yatima na wajane, mojawapo ni kufa mapema, watoto wako kubaki mayatima na ongezeko la wajane kwenye kizazi chako, katika kitabu hiki nimeeleza kwa kina sana haya yote. **MUHIMU KUJUA:** Mungu hamuelewi mtu yoyote anayetoa sababu za kushindwa kuwasaidia wajane na yatima au wahitaji.

Kwa maoni, ushuhuda na ushauri tuwasiliane kwa simu ya mkononi 0682216630 au 0655300010

Barua pepe: emmanuelphilipo2000@gmail.com